

## **UGONJWA WA UNYAYO MGUMU WA MBWA (CANINE DISTEMPER OR HARDPAD DISEASE)**

### **Na Augustino Chengula**

Huu ni ugonjwa wenyе maambukizi makubwa na hivyo huenea kwa njia ya hewa na matone ya makamasi na hushambulia mfumo wa upumuaji, chakula na zaidi sana mfumo wa fahamu kwa mbwa wadogo na wakubwa. Dalili kuu za ugonjwa huu ni homa mbili, kupungua kwa chembe hai nyeupe, kutoka makamasi mengi na mate mdomoni, vichomi vyа marа kwa marа, na matatizo ya mfumo wa fahamu (kizunguzungu, kushindwa kutembea, kuanguka chini) na unyayo pamoja na pua huwa ngumu.

Ugonjwa huu hutokea kwa wanyama jamii ya mbwa (mbwa, mbweha na mbwa mwitu), nguchiro na kicheche. Hivyo kwa wanyama wa kufugwa ni umwa pekee mwenye uwezo wa kuupata ugonjwa huu.

### **Kisababishaji na ueneaji wake**

Virusi aina ya *paramyxovirus* ndio wanababisha ugonjwa huu na njia kuu ya maambukizi ni kuitia njia ya hewa na majimaji ya mfumo wa fahamu (makamasi) wa mbwa mwenye ugonjwa. Lakini pia kwa vile ugonjwa huwapata mbwa pori, mwingiliano kati ya mbwa wa kufugwa na wale wa porini husabisha kuenea kwa ugonjwa. Mbwa wote wanaweza kupata ugonjwa huu lakini hatari kubwa ni kwa mbwa wadogo wenyе umri wa miezi chini ya 4 na wale ambaо hawajachanjwa dhidi ya ugonjwa huu.

### **Dalili za ugonjwa**

**Homa ya 1:** Hii ni homa ya mpito na mara nyingi hutokea siku 3-6 tangu maambukizi na dalili zinaweza kupita bila ya kutambuliwa na mwenye mbwa. Kisha homa hii hupotea siku chache baadaye.

**Homa ya 2:** Hii hutokea mara baada ya homa ya kwanza na hupotea si zaidi ya wiki 1 tangu ianze. Dalili zinazotambulisha ugonjwa huu huwa kwenye homa hii ya pili nazo ni kama zinavyoonekana hapa chini.

-Mbwa huanza kutiririsha machozi ya majimaji na baadaye mazito mithili ya usaha

**-Mfumo wa upumuaji/hewa** (kutiririka kwa mafua mepesi na kukoho)

**-Mfumo wa chakula** (kupoteza hamu ya kula, kutapika, kuharisha, kuchoka,na kukosa nguvu).

-Unyayo wa mbwa na pua vyaweza kuwa vigumu (Hyperkeratosis)-asili ya jina la ugonjwa-**ugonjwa wa unyayo mgumu**.



**-Dalili za mfumo wa fahamu** (kizunguzungu, kucheza cheza kwa nyama maeneo kadhaa ya mwili mfano miguuni na mashavuni, kupooza mwili mara nyingi huanzia miguu ya nyuma kisha mwili wote, , kutiririsha mate na kuchezesha taya mfano wa

kutafuna kitu mdomoni). Kizunguzungu kikizidi mbwa huanguka chini huku ***akichezesha miguu mithili ya kuendesha baiskeli***, kukojoa na kunya bila ya kujitambua. Ugonjwa ukikomaa zaidi kichwani hupelekea mbwa kukandamiza kichwa chini/kwanye vitu vigumu au huendelea kupiga hatua.



Muda wa dalili za mifumo yote ya mwili yaweza kuwa siku 10, lakini zile za mfumo wa fahamu zinaweza kuchukua siku nyingi zaidi.

### **Utambuzi wa ugonjwa**

Ugonjwa huu unaweza kutambuliwa kwa kutumia dalili zilizotajwa na vipimo vya maabara.

### **Matibabu na Kinga**

Hakuna matibabu maalumu yanayoweza kuua virusi kwa mbwa na hivyo matibabu yatategemea dalili zinazojitokeza ili kuzuia maambukizi pili ya bakteria, kuzuia huharisha, kutapika pamoja na dalili za mfumo wa fahamu. Mbwa wagonjwa wanatakiwa wapewe matunzo ikiwa ni pamoja na kuwekewa mazingira ya joto, chakula kizuri na kutengwa kutoka mbwa wengine.



Mbwa aliyefungwa maski kuzuia asieneze ugonjwa kupitia mtiririsho wa mate na makamasi

Kuchanja mbwa pamoja na kuzuia mbwa wasikutane na mbwa wenyewe ugonjwa ni vitu vya muhimu sana kuwakinga mbwa na ugonjwa. Chanjo ni muhimu sana hivyoanza kuchanja mbwa wako wakiwa wadogo kuanzia umri wa wiki 6-8 na kisha kati ya wiki 2-4 hadi wawe na wiki 16, baada ya hapo chanja kila mwaka.



Chanjo inayokinga magonjwa matatu (distemper, adenovirus [hepatitis],

parainfluenza, and parvovirus - DHPP)